

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA

15 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 15 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa

Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

339. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Muleba.

340. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Kisasa katika Kata ya Kiwira – Rungwe.

341. MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, TARURA ina mpango gani wa kujenga Barabara kwenye kona kali na Milimani kwa kutumia zege katika Jimbo la Lushoto.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

342. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapandishia Mishahara Wafanyakazi.

WIZARA YA FEDHA:

343. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, mikopo kiasi gani imetolewa na Taasisi za Fedha kwa dhamana ya mali zilizorasimishwa na Wanawake wangapi wamenufaika.

344. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itaweka Kituo Kidogo cha Forodha katika Kata ya Itoryo/Bikonge pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kupata bidhaa toka Kenya.

WIZARA YA KILIMO:

345. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, upi mpango wa kuwasaida Wakulima wa Tumbaku kupata vitendea kazi mapema na kupunguza bei vikiwemo *Jute Twine* na *Cotton Twine*.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

346. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kujenga kiwanda cha kuchakata Samaki katika Ukanda wa Bahari ya Hindi.

WIZARA YA UCHUKUZI:

347. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina Mpango gani wa kudhibiti Mabasi yanayokwepa kuingia Stendi na kushusha Abiria Barabarani.

WIZARA YA MAJI:

348. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza changamoto ya maji Wilaya ya Nkasi.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

349. MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO (MBARALI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanga matumizi bora ya ardhi kutokana na kasi ya ongezeko la Watu nchini.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA
YA HABARI:**

**350. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la Mtandao wa Simu
kwenye baadhi ya maeneo katika Jimbo la Tabora
Mjini.

**351. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX
(BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mkakati gani ya kukomesha wizi wa
mtandaoni.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya
Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha
2024/2025.

**DODOMA
15 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**